

## **DHAMBI SABA ZA KUFISHA**

### **Na Christopher Mwakabanje**

#### **SEHEMU 1**

Katika Mithali 6:16-19 machukizo saba yanetajwa yanayomwudhi Mungu. Hatuwezi kutilia maanani namba saba, kwani Sulemani angeweza kuorodhesha zaidi ya vitu hivyo, lakini hapo ametoa taswira kamili ya jinsi Mungu anavyoyachukia maovu yote. Ni sawa na kusema machukizo hayo sita ni mabaya, lakini yakifika saba ni kilele cha ubaya wote. Mtu mwenye tabia kama hizo hafai kitu, ni mwovu (Mith.6:12).

Sulemani ametumia mtindo kama huo pia katika Mithali 30:18-24 akisema, “*Kuna mambo matatu yaliyo ya ajabu kwangu, Naam, kuna manne nisiyoyafahamu... Kwa ajili ya mambo matatu nchi hutetemeka, Naam, kwa ajili ya manne haiwezi kuvumilia.*” Nabii Amosi katika 1:3 pia anasema, “...*Kwa makosa matatu ya Dameski, naam, kwa manne, sitaizuia adhabu yake isimpate...*” (linga. Amosi 1:6,9,11,13; 2:1,4,6). Ni sawa na kusema kwa makosa matatu ningevumilia, lakini kwa manne hata siwezi kuvumilia nighairi hukumu juu yao.

#### **ULIMI WA UONGO**

Machukizo matatu kati ya hayo saba husababishwa na ulimi: (1) ulimi wa uongo, (2) shahidi wa uongo na (3) kupanda mbegu za fitina kati ya ndugu. Ingawa ulimi unaweza kutumika katika kujenga, unaweza pia kuleta madhara makubwa sana ukitumiwa vibaya.

Akizungumzia kuhusu ulimi Yakobo anasema, “*Nao ulimi ni moto; ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viingo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huuwashwa moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanum*” (Yak.3:6).

Mungu ni mkweli daima na ndani yake hakuna uongo, lakini kinyume chake tunasoma, “*Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo*

” (Yoha.8:44). Ni rahisi kwa wanadamu kuutambua uongo mara moja ukinenwa dhidi yake, walakini ni vigumu kwa wanadamu wengi kuutambua uongo unaponenwa dhidi ya Mungu. Kwa kuwa watu wengi hawajui wala hawasomi Neno la Mungu, basi hawatofautishi uongo na ukweli katika masuala ya imani. Ni jambo la kawaida katika ulimwengu wa madhehebu kunena na kufundisha mambo ambayo Mungu hajawahi kunena. “*Usiongeze neno katika maneno yake; asije akakulaumu, ukaonekana mwongo*” (Mithali 30:6).

Nabii kijana alikuwa na ujasiri wa kutosha kusema ukweli mbele ya Mfalme Yeroboamu, walakini alidanganywa na nabii mzee. “...*Mimi nami ni nabii kama weve, na malaika akaniambia kwa neno la BWANA, kusema, Mrudishe pamoja nawe nyumbani kwako, ale chakula, akanywe maji, lakini alisema uongo*” (1 Wafalme 13:18). Pia, tukidai tu kwa vinywa vyetu kwamba tunamjua Bwana, walakini tusitende anayotuamuru kuyatenda tutakuwa tunasema uongo (1 Yoh. 2:4).

#### **USHAHIDI WA UONGO**

Amri ya kutoshudia uongo ni kati ya Amri Kumi za torati (Kut.20:16). Katika kesi za mauaji (Hesabu 35:30; Kumbukumbu 17:6) mashahidi wawili au watatikia kutoa

ushahidi kabla ya adhabu ya kifo kutolewa. Mungu alikataza ushahidi wa mtu mmoja (Kumb.19:15-18). Ikiwa shahidi alitoa ushahidi wa uongo alitakiwa kupata adhabu kulingana na kosa alilolitolea ushahidi. “*Shahidi wa uongo hakosi ataadhibiwa; wala asemaye uongo hataokoka*” (Mith.19:5). Sheria ya jicho kwa jicho, jino kwa jino, ilitumika kwa shahidi wa uongo pia (Kut.21:23; Lawi 24:20).

Yesu alitafutiwa mashahidi wa uongo na viongozi waliopotoka, akahukumiwa kifo (Mathayo 26:59-61). Maneno yetu yanapaswa kuwa ndio, ndiyo; au siyo, siyo; kwa maana yazidio hayo yatoka kwa yule mwovu (Mathayo 5:37).

### **MBEGU ZA FITINA**

Kupanda mbegu za fitina ni kuleta ugomvi, ufisadi, chuki, uchongezi, n.k., kati ya ndugu. Fitina huleta kutolewana kati ya ndugu kama ilivyokuwa katika kanisa la Korintho (1:10-13). Kanisa kupewa majina ya wanadamu ni kuleta fitina na kuligawa kanisa la Bwana. Mtu asiyefaa, hupanda mbegu za magomvi kati ya ndugu (Mithali 6:14). Tujitahidi daima kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani (Efe.4:3; linga. Rum. 6:18; Math. 5:9; Waeb. 12:14). “*Moto hufa kwa kukosa kuni, na bila mchongezi fitina hukoma. Kama makaa juu ya makaa yanayowaka, na kama kuni juu ya moto; ndivyo mtu mgomvi achocheaye uadui*” (Mithali 26:20-21).

### **MASWALI**

1. Machukizo matatu kati ya saba husababishwa na ulimi; yataje hayo matatu.
  - a) \_\_\_\_\_
  - b) \_\_\_\_\_
  - c) \_\_\_\_\_
2. Tunaweza kunena uongo dhidi ya \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_.
3. Yesu alipohukumiwa viongozi wa dini walitafuta ushahidi 2ain? Na ni adhabu ipi wangestahili kupewa kutokana na ushahidi huo? Toa fungu la Maandiko.
4. Baba wa uongo ni nani? \_\_\_\_\_
5. Eleza jinsi kanisa la Korintho lilivyoleta fitina mionganini mwao.
6. Je, idadi ya mambo anayoyachukia Mungu ni sabu tu? \_\_\_\_\_
7. Hatuwezi kuleta fitina tukiligawa na kuliita kanisa la Kristo kwa majina ya wanadamu?  
\_\_\_\_\_

